**MALENGO NA NIDHAMU YA MATUMIZI YA FEDHA YAKOMBOA KAYA MASKINI**

**Bi Justina MwalaLutonjo** mwenye umri wa miaka 38 ni Mkaziwa Kijiji cha Usevya ana watoto 3 watoto wawili (2) wanasoma na motto mmoja (1) hasomi Bi Justina anapokea kiasi cha Tshs. 36,000.00




Maisha baada ya kuanza kupokea fedha za kunusuru Kaya Maskini Bi Justina anasema anaishukuru Serikali kwa kuanzisha mpango wa kunusuru Kaya Maskini kwa kuwapatia

fedha kwani imemsaidia kuboresha maisha yake na ameweza kujenga nyumba ya kudumu ambapo kabla hakuwa na uwezo wala ndoto za kuweza kujenga nyumba ya kudumu kama inavyoonekana hapa chini.



Matarajio yake ni kuanzisha shughuli za kilimo na biashara kwakufanya shughuli za ufugaji wa Ng'ombe na Nguruwe pia anishauri Serikali kuendelea kusaidia zaidi wananchi kama wanavyoendelea kusaidia kwa sasa.

**Bi Esther Kashinje** mwenye umri wa miaka 50 ni mkazi wa Kijiji cha Usevya ana watoto **9** watoto watatu **(3)** wanasoma wengine sita **(6)** hawasomi ni moja kati ya Kaya Maskini zinazonufaika na fedha za kunusuru Kaya Maskini **(TASAF)** tangu mwaka 2014 baada ya mume wake kufariki

**Bi Esther Kashinje**anasimulia kuwa aliishi maisha magumu kabla ya kaya yake kuingizwa kwenye mpango wa kunusuru Kaya Maskini ambapo alikuwa akipata mazingira magumu katika kupata chakula na malazi kama nyumba yake inavyoonekana hapa chini.






**Bi Esther Kashinje**anasimulia kuwa baada ya kuingizwa kwenye mpango wa Kunusuru Kaya Maskini amefanikiwa kwa kiasi kikubwa kwani ameweza kujenga nyumba ya kudumu kama inavyoonekana hapa chini na kuanzisha shughuli za ushonaji wa nguo, kazi ambayo inamwingizia kipato na kupata chakula kwa ajili ya familia kama inavyoonekana hapa chini.




**Bi Esther Kashinje**Mradi wa kunusuru Kaya Maskini umemwezesha kuanzisha shughuli ya ufugaji ambapo ameweza kuanzisha ufugaji wa Mbuzi na Nguruwe na kumwezesha kupeleka Watoto na Wategemezi wengine Shule baada ya kuwa na uwezo wa kupata mahitaji ya Wanafunzi kama kununua daftari na Sare za Shule kama inavyoonekana hapa chini.

**Ufugaji wa Mbuzi**




**Ufugaji wa Nguruwe**




**Bi Esther Kashinje** anamatarajio ya kuinua zaidi shughuli za kilimo ambapo anaeleza kuwa atajikita katika shughuli za kufuga Ng'ombe, Mbuzi  na Nguruwe ambapo mifugo anaeleza kuwa mifugo hiyo itamsaidia katika kununua mahitaji ya Wananchi na Ushauri Serikali kuendelea kubaini na kusaidia Kaya nyingi zaidi katika jamii anamoishi.

**Bwana Ephraimu Ilumba** mwenye umri wa miaka 50 Mkazi wa Kijiji cha Ikuba mwenye Watoto wawili (2) wote wanasoma mmoja darasa la kwanza (I) na mwingine darasa la pili (II) anaeleza kuwa kabla ya kuingizwa kwenye mpango wa Kunusuru Kaya Maskini alikuwa na maisha duni kwani alipata huduma ya mlo mmoja kwa siku wakati

mwingine kukosa kabisa chakula, alikuwa napata huduma duni ya Afya na mazingira duni ya makazi.

**Bwana Ephraimu Ilumba** anaeleza kuwa amepata mafanikio makubwa baada ya kuingizwa kwenye Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini kwani ameweza kujenga nyumba na kuanzisha shughuli ya ufugaji wa Nguruwe na kupeleka watoto wote Shuleni kama inavyoonekana hapa chini.




09 03 2018


09 03 2018

**Bwana Ephraimu Ilumba** anashauri kuwa wanufaika wote wa Mradi wa TASAF wenye lengo la kunusuru Kaya Maskini wazingatie kujenga nyumba za kudumu badala ya kuelekeza fedha hizo kwenye matumizi yasiyotekeleza malengo ya kuanzishwa kwa mradi na kueleza kuwa anamalengo ya kujenga nyumba ya kudumu kwani tayari anabati 25 ndani ya nyumba anayoishi kwa sasa ili ajikwamue na maisha ya kuishi kwenye nyumba za makuti.

Bi Monica Wankumba mwenye watoto wawili wote wanasoma ni mkazi wa Kijiji cha Ikuba anapokea Tshs. **20,000.00**anaeleza kuwa kabla ya kuingizwa kwenye mpango wa kunusuru Kaya Maskini alikuwa na maisha duni kwanialikuwa na nyumba duni na baada ya kuingizwa kwenye mpango mwaka 2014 ameweza kujenga nyumba ya kudumu kama inavyoonekana hapa chini.

**Nyumba Kabla ya kuingia kwenye Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini**




**Nyumba ya Kuingizwa kwenye Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini**




**Bi. Elizabeth Mabula Nyanda mwenya umri wa miaka 57** ni mkazi wa Kijiji cha Ilalangulu ana watoto watatu (3) wote wanasoma Shule anaeleza kuwa kabla ya kuingia kwenye mpango wa kunusuru Kaya Maskini alikuwa na maisha duni tofauti na alipoingizwa kwenye mpango ameweza kuanzisha miradi ya ufugaji wa Mbuzi kununua shamba analofanya shughuli za kilimo na kujenga Nyumba ya Kudumu kama inavyoonekana hapa chini.

**Makazi kabla ya kuingizwa kwenye mpango wa kunusuru Kaya Maskini**



**Ufugaji wa Mbuzi baada ya kuingizwa kwenye Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini**



**Shughuli za Kilimo baada ya kuingizwa kwenye Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini**



**Makazi baada ya kuingizwa kwenye mpango wa Kunusuru Kaya Maskini**




**Bi. Elizabeth Mabula Nyanda** anashauri wanufaika wote wa mradi wa Kunusuru Kaya Maskini waelekeze nguvu katika kuwekeza na kuibua miradi mbalimbali itakayowasaidia kujipatia mahitaji ya siku kwenye kaya zao na Serikali iendelee kusaidia wananchi wake hususani wanaoishi katika mazingira magumu na kupata mahitaji duni.

**Bi Jalasia Kaposa** mwenye umri wa miaka 53 ni mkazi wa Kijiji cha Ilalangulu Kata ya Kibaoni hana mtoto hata mmoja anapokea kiasi cha Tshs. 20,000.00 anasimulia kuwa kabla ya kuingia kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Jamii TASAF alikuwa akiishi maisha duni kwa kukosa lishe bora, kuishi kwenye duni na Afya duni lakini baada ya kuingizwa

kwenye mpango wa kunusuru Kaya Maskini alifanikiwa kuboresha maisha kwa kuwa na uwezo wa kupata mahitaji ya kila siku kwenye Kaya yake kama inavyoonekana hapa chini.

**Bi Jalasia Kaposa** kabla ya kuingizwa kwenye mpango wa kunusuru Kaya Maskini alikuwa na makazi duni kama inavyoonekana hapa chini.




**Bi Jalasia Kaposa** amefanikiwa kujenga nyumba bora baada ya kuingizwa kwenye mpango wa kunusuru Kaya Maskini pia amefankiwa kuanzisha mradi wa ufugaji wa Ng’ombe ambapo mpaka sasa amefanikiwa kufuga Ng’ombe aina ya maksai wanne kama inavyoonekana hapa chini.

**Makazi ya Bi Jalasia Kaposa baada ya kuingizwa** kwenye mpango wa kunusuru Kaya Maskiniamefanikiwa kujenga nyumba ya kudumu kama inavyoonekana hapa chini.




**Bi Jalasia Kaposa** baada ya kuingizwa kwenye mpango wa kunusuru Kaya Maskini amefanikiwa kuanzisha mradi wa ufugaji ameweza kufuga mifugo mbalimbali Ng'ombe ambapo amefanikiwa kufuga maksai wanne kama inavyoonekana hapa chini.




**Bi Angel Athanaz Lyoba** Mkazi wa Kijiji cha Kibaoni ana Watoto wanne (4) wote wanasoma Shule anapokea Tshs. 40,000.00 anasimulia kuwa kabla ya kuingia mpango wa kunusuru Kaya Maskini alikuwa na maisha duni alikuwa anashindwa kupata mahitaji yake ya msingi katika Kaya na kupata mahitaji ya watoto wanapotakiwa kuhudhuria masomo.

Lakini anaelezea kuwa baada ya kuingia kwenye mpango wa kunusuru Kaya Maskini watoto wanapata mahitaji ya Shule kama daftari na kalamu kwa wakati na kuhudhuria Shuleni kila siku za masomo na ameweza kuanzisha mradi wa ufugaji ambapo ana nguruwe kama inavyoonekana hapa chini.

Makazi kabla ya kuingia kwenye mpango wa kunusuru Kaya Maskini yalikuwa duni kama inavyoonekana hapa chini




Maisha baada ya kuingia kwenye mpango wa kunusuru kaya Maskini ameweza kuanzisha mradi wa ufugaji wa Nguruwe kama inavyoonekana hapa chini.

